

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI



TANGAZO LA UWAKALA WA KUKUSANYA USHURU
WA MAZAO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali inakaribisha maombi ya kuwa wakala wa ukusanyaji mapato ya Halmashauri kwa kipindi cha Mwaka 2017/2018 kutoka kwa wazabuni wenye sifa za kufanya kazi hiyo kwa vyanzo vifuatavyo:-

1. USHURU WA MAZAO LGA/2017-2018/076/R/01
 - Lot 1 Kanda A** - Inajumuisha Kata za Madibira na Miyombweni.
 - Lot 2 Kanda B** - Inajumuisha Kata za Ipwani, Igava, Rujewa, Lugelele, Imalilo Songwe, Mawindi na Ubaruku na Mbarali Estate
 - Lot 3 Kanda C** - Inajumuisha Kata za Ihahi, Itamboleo, Chimala, Mapogoro na Kapunga Rice Farm.
 - Lot 4 Kanda D** - Inajumuisha Kata za Utengule Usangu, Luhanga, Mwatenga, Mahongole, Ruiwa na Kongolo Mswiswi na Igurusi (nje ya soko).
1. Ushuru wa mnada wa Utengule Usangu LGA/2017-2018/076/R/02
2. Ushuru wa mnada wa Imalilo songwe LGA/2017-2018/076/R/03
3. Ushuru wa mnada wa Ukwavila LGA/2017-2018/076/R/04
4. Ushuru wa mnada wa Mapogoro LGA/2017-2018/076/R/05
5. Ushuru wa mnada wa madibira LGA/2017-2018/076/R/06
6. Ushuru wa mnada wa Igava LGA/2017-2018/076/R/07
7. Ushuru wa mnada wa Rujewa LGA/2017-2018/076/R/08
8. Ushuru wa masoko kata Mahongole, Ruiwa, Mwatenga na Kongolo mswiswi LGA/2017-2018/076/R/09
9. Ushuru wa masoko kata za Chimala, Igurusi, Utengule usangu, Itamboleo na Mapogoro LGA/2017-2018/076/R/10
10. Ushuru wa masoko kata za Ubaruku, Rujewa, Imalilo Songwe, Lugelele, Igava, Mawindi, Ipwani, Madibira na Miyombweni LGA/2017-2018/076/R/11

MASHARTI YA MAOMBI:-

1. Mwombaji awe na Leseni ya Biashara, TIN, Hati ya Usajili, Utambulisho (Power of Attorney) na pia awe na ofisi inayotambulika (ataje ofisi ilipo, anuani, namba ya simu na fax kwa ajili ya mawasiliano).
2. Mwombaji awe tayari kuweka dhamana ya malipo ya miezi mitatu ambayo ni Dhamana ya Benki (Bank Guarantee) au fedha taslimu.
3. Mwombaji awe tayari kutumia viwango vilivyowekwa na Halmashauri na atumie Sheria ndogo ya Ushuru wa Mazao GN 363 ya tarehe 04/10/2013 ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.

4. Mzabuni atatumia mfumo wa kielektoni kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri.
5. Mzabuni atatakiwa kuwasilisha makusanyo yote ya siku kwenye akaunti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri.
6. Mzabuni atarudishiwa asilimia kumi na mbili nukta tano (12.5%) ya makusanyo yote kila mwezi.
7. Waombaji wanaweza kuwa watu binafsi, Kampuni, Shirika au Kikundi cha watu waliosajiliwa kisheria.
8. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.
9. Mwombaji haruhusiwi kuweka alama yoyote ya utambulisho wake juu ya bahasha.
10. Mwombaji aambatanishe idadi ya kazi za ukusanyaji mapato na vielelezo (Kama vile: Barua ya kuteuliwa kuwa wakala, Fomu ya makubaliano ya Mkataba) ailizowahi kufanya na uwezo wa kifedha (financial capacity) – Bank Statement ya miezi mitatu ya Marchi, Aprili na Mei 2017.
11. Mwombaji ataruhusiwa kuomba zaidi ya zabuni moja kwa kutumia maombi kwenye bahasha tofauti. Juu ya bahasha iandikwe kwa **HERUFI KUBWA** namba ya zabuni aliyoomba, aina ya zabuni, namba ya loti na ifungwe kwa **LAKIRI (SEAL)** na maombi yakiambatana na kivuli cha Stakabadhi ya ada ya maombi yaletwe kwa

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI,
S. L. P 237
RUJEWANA - MBEYA.**

12. Vitabu vya zabuni kwa lugha ya Kiswahili vinauzwa kwa Tshs 50,000/= ambazo hazitarudishwa kwa mwombaji na vinapatikana katika Ofisi ya, **Afisa Ugavi (W), Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, S. L. P 237, Rujewa - Mbeya.**
13. Malipo yote yafanyike kupitia **Bank ya NMB, Akaunti ya Own source Collection, Akaunti Namba. 61110000719** na Slip ya Bank iletwe kwa Mhasibu ili upatiwe risiti kuanzia saa **02.00 asubuhi hadi saa 09:30 alasiri siku za kazi.**
14. Maelezo ya ziada (Masharti) yatapatikana kwenye kitabu cha zabuni husika.
15. Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali hailazimiki kukubali au kukataa ombi lolote.
16. Mwombaji anashauriwa kabla ya kuomba Zabuni yoyote kufanya utafiti wa kutosha.
17. Mwombaji anaweza kuja Ofisi za Halmashauri kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kupata uafanuzi atakaohitaji ikiwa ni pamoja na kuonyeshwa sehemu za kukusanyia mapato.
18. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni **09/06/2017 saa 05:00 asubuhi** na zabuni zitafunguliwa siku hiyo hiyo **saa 05:01 asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya.** Waombaji au wawakilishi wao wanakaribishwa kuhudhuria siku ya ufunguzi.

.....
Kivuma H. Msangi,
MKURUGENZI MTENDAJI (W),
MBARALI.